

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Barua Pepe: ps@mit.go.tz
Barua Pepe: gc@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
Nukushi: +255262963117



Mji wa Serikali, Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S.L.P 2996,
40478, Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZA MUDA WA KUWASILISHA TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA
WA KAMPUNI (BENEFICIAL OWNERS)

4 Januari, 2022, DODOMA.

1. Kuhusu Umiliki Manufaa Katika Kampuni

Kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, ili kampuni iweze kufanya biashara nchini inapaswa kusajiliwa na Wakala wa Usajili wa Makampuni na Biashara (BRELA). Ili kupata usajili, pamoja na mambo mengine, wahusika hupaswa kuwasilisha taarifa mbalimbali ikiwemo majina na wasifu wa wamiliki na wanahisa wa kampuni husika. Kwa mujibu wa Sheria hii, taarifa za kampuni huwekwa wazi katika daftari ya msajili na mtu yeyote anaruhusiwa kupekua daftari kama anahitaji kupata taarifa za kampuni husika.

Hata hivyo, hapo awali wamiliki wa kampuni walikuwa hawalazimiki kuwasilisha taarifa za ziada za wanufaika wengine wa kampuni. Uzoefu unaonesha kuwa majina yanayowasilishwa katika usajili wa kampuni ni majina ya waendesha kampuni na wakati mwingine majina ya wamiliki halisi na wanufaika wakubwa wa kampuni hizo hayapo katika daftari la msajili. Mmiliki Manufaa ni mtu ambaye sio lazima aonekane kwenye nyaraka za makampuni lakini anamiliki, anafanya maamuzi, anahodhi au anaendesha asilimia kubwa ya uwekezaji kwenye kampuni au makubaliano ya kibiashara. Aidha, Benki ya Dunia na Taasisi nyingine za Kimataifa zinazohusika na masuala ya biashara zimesisitiza umuhimu wa kuongeza uwazi na uwajibikaji katika umiliki wa makampuni, ikiwemo kutambua wamiliki halisi wa manufaa katika kampuni.

2. Marekebisho ya Sheria ili Kupata Taarifa za Wamiliki Manufaa

Kama sehemu ya juhudi za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, na katika kuendelea kukabiliana na uhalifu wa kiuchumi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Sheria ya Fedha, 2020 (*Finance Act, 2020*) lilipitisha marekebisho ya Sheria ya Makampuni, Sura ya 212 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa (*Beneficial Owners*) katika kampuni zilizosajiliwa hapa nchini.

Katika kutekeleza marekebisho haya ya Sheria, Kifungu cha 459A cha marekebisho hayo, kilizitaka Kampuni zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni kuanza kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa (*Beneficial Owners*). Kanuni za kutekeleza Sheria hii zilikamilika Mwaka jana mwezi Mei na makampuni yalipewa miezi sita yawe yamewasilisha taarifa hizo. Hata hivyo, kutokana na upya wa dhana ya Umiliki Manufaa, makampuni mengi hayakuweza kuwasilisha taarifa zao na yameleta maombi ya kuongezewa muda. Hadi tarehe 3 Januari, 2022 ni makampuni 14,026 pekee yameweza kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa kwa Msajili wa Makampuni, ambayo ni sawa na asilimia 14 ya matarajio.

3. Kuongeza Muda wa Kuwasilisha Taarifa za Wamiliki Manufaa

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, na kwa kuzingatia maombi ya wafanyabiashara wengi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha taarifa husika, na kwa mamlaka niliyo nayo kwa mujibu wa Kifungu cha 459A (2) cha Sheria ya Makampuni, Sura ya 212, nimeamua kuongeza muda wa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa (*Beneficial Owners*) kwa muda wa miezi sita (6) kuanzia tarehe 1 Januari, 2022.

Ninaielekeza BRELA itumie nafasi hii kuendelea kutoa elimu na kuhamasisha umma na wamiliki wa Kampuni kuhusu dhana, umuhimu na faida za kuwasilisha taarifa za umiliki manufaa. Aidha, ninawahimiza wamiliki wa makampuni wote kutekeleza matakwa ya Sheria niliyoyataja hapo juu ndani ya kipindi hiki cha nyongeza.

Prof. Kitila Mkumbo (Mb),
WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA